# IMAM ALI
# NA
# MFUMO WA USAWA

الإمام على و نـهج المساواة

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa as-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepitiwa na:**
Mbaraka A. Tila

ترجمة

# الإمام علي و نهج المساواة

تأليف

الشيخ حسن الصفار

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

بسم الله الرحمن الرحيم

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 - 9987 – 17 – 050 – 0

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa as-Safar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul Karim Juma Nkusui
**Barua pepe:** abdulkarimjuma@yahoo.com

**Kimepitiwa na:**
Mbaraka A. Tila

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Januari, 2014
**Nakala:** 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ........................................................ 01

Utangulizi ........................................................ 03

Ali na Malezi ya Nabii ........................................................ 05

Ali ana Cheo Sawa na Harun (as) ........................................................ 09

Hadith ya Cheo ........................................................ 13

Malezi na Maandalizi ........................................................ 16

Mfumo wa Usawa ........................................................ 18

Ubaguzi, Hatari na Madhara ........................................................ 21

Baina ya Yaliyopita na Yaliyopo ........................................................ 22

Uislamu ni Sharia ya Usawa ........................................................ 26

Mfumo wa Usawa ........................................................ 28

Usawa Katika Kutoa ....................................................................30

Haki za Wasiokuwa Waislamu......................................................36

Pamoja naWapinzani wa Rai.........................................................38

Muamala wa Kibinadamu Katika Sira ya Imam Ali.....................40

Maji ni Haki ya Wote ...................................................................42

Hata Mhaini ana Haki Zake ..........................................................45

Kuchukia Kuadhibu .....................................................................48

Kumfanyia Wema Mhalifu...........................................................49

Au Kusamehe Dhambi.................................................................51

Bibliografia ..................................................................................51

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjuma ya Kiswahili ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho, “الإمام على و نهج المساواة ”. Sisi tumekiita, Imam Ali na Mfumo wa Usawa.

Imam Ali (a.s) alikuwa Khalifa wa nne kama anavyotambulika kwa Waislamu wote, lakini yeye pia ni Imam wa kwanza katika mlolongo wa Maimamu 12 wanaotokana na Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) wanaofuatwa na Waislamu wa madhehebu ya Shia Ithnaasharia.

Mwandishi amekiita kitabu chake hiki, *Imam Ali na Mfumo wa Usawa* si kwa sababu nyingine bali ni kwa sababu ya jinsi Imam Ali (a.s.) alivyotawala kwa uadilifu, hekima na busara kubwa wakati wa utawala wake. Amesifiwa hivyo na wote - maadui na marafiki. Na kila mwenye kufuatilia historia ya Uislamu hili hawezi kulipinga.

Madhumuni ya kitabu hiki ni kujaribu kuwaonesha watawala wa zama hizi na zinazokuja mfano wa utawala wa Imam Ali (a.s.) uliosimama juu ya misingi ya uadilifu, usawa na haki. Hii ni kwa sababu Imam Ali ni Mlango wa elimu ya Mtume (s.a.w.w.) pale aliposema: “Mimi ni jiji la ilmu na Ali ni mlango wake.” Hivyo, mtu hawezi kushangaa anaposikia Imam Ali anaposifiwa kwa sifa hii - ni stahiki yake.

Sisi tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya kielimu ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni

yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Alhaji Abdul-Karim Juma Nkusui kwa kazi kubwa aliyofanya ya kukitarjumi kwa lugha ya Kiswahili, pia na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

# UTANGULIZI

بسم الله الرحمن الرحيم

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu**
**Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.**

Ummah wa Kiislamu unahitaji katika zama hizi kisimamo kirefu na tafakari ya kina, ili kurejesha mfumo wa uhusiano wake wa ndani baina ya nguvu na makundi mbalimbali ya kijamii. Wakati ambapo watu wengi ulimwenguni wameboresha hali yao ya kijamii katika upande wa kuheshimu Haki za Binadamu na kutegemea Mfumo wa Demokrasia na ushirikishwaji wa raia, bado raia wa nchi za Kiislamu wanateswa chini ya mbinyo wa ukandamizaji, na wanakabiliwa na mateso ya ubaguzi wa utaifa, makundi na ukabila, uvunjifu wa Haki za Binadamu na mdororo wa usalama wa kijamii, kwa ukosefu wa utulivu na uhusiano mzuri baina ya mielekeo na makundi mbalimbali.

Na sababu za hali hii ya kutoendelea zinarejea katika urithi wa kihistoria na ada ya kiutamaduni, kwani pamoja na kwamba Ummah unamiliki ujumbe bora zaidi wa Mwenyezi Mungu, na mfumo kamilifu zaidi wa maisha ambao unaonekana katika misingi ya Kiislamu na mafunzo yake, isipokuwa bado utekelezaji mbaya wa mfumo huu, ukiukwaji wa misingi ya ujumbe ambao umefunika sehemu kubwa zaidi ya historia ya Ummah kasoro zama za utume, zama za ukhalifa wema na baadhi ya maeneo, bado umeuelemea uti wa mgongo wa Ummah kwa mzigo mzito kwa mbeleko ya urithi na ada zisizo sahihi, ambazo zimeutoa ujumbe wa Kiislamu katika ma-

lengo yake ya kijamii na zimeukosesha hadhi yake ya ubinadamu, na zimeubadilisha na kuwa mkusanyiko wa ibada na mazingatio ya kiibada, na kuudhalilisha kwa ajili ya visingizio vya kuhalalisha hali ya ukandamizaji na kuhami mila na ada zisizo na maendeleo.

Na kwa ajili ya kuvuka urithi na ada hizi nzito, ni lazima turejee kwenye chemchem safi ya Kiislamu na maarifa yake ya asili ili Ummah uchukue kutoka humo roho ya maboresho na maendeleo, na ili urejeshe muundo wa uwepo wake na mfumo wa uhusiano wake kwa mwanga wa uongofu wa wahyi wa Mwenyezi Mungu, ambao umekuja kumtoa mwanadamu kwenye giza na kumpeleka kwenye nuru, na kumkomboa mwanadamu kutokana na minyororo na pingu zote, na kutengeneza jamii adilifu na yenye usawa.

Ali bin Abu Talib (as) katika kauli zake na vitendo vyake, baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) anawakilisha sura nzuri na mfano mzuri kwa ajili ya kubainisha uongofu wa Kiislamu, na kutekeleza maadili yake na mafunzo yake katika kujenga jamii na mfumo wa uhusiano wake. Na kurasa hizi chache zinajaribu kuelekeza kiasi kidogo tu miongoni mwa fikra za Ali na sira yake katika kuimarisha mfumo wa usawa baina ya wanajamii na kutatua tatizo la ubaguzi ambao umechosha jamii nyingi za kibinadamu katika wakati uliopita na uliopo.

**Hasan Safar**
**8/7/2003 Miladiyya,**
**8/5/1424 Hijiria.**

# ALI NA MALEZI YA NABII (SAWW)

Kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu, kuwakomboa binadamu kutokana na ujahili na shirki, na kuwatoa wao katika giza na kuwapeleka kwenye nuru, ni kazi ngumu sana, ni jukumu kubwa sana na hiyo ni kwa sababu ya ugumu wa kubadilisha mielekeo na ada zilizorithiwa zilizojikita katika nafsi za watu na nyendo zao, hususan wakati zinapochukua sifa ya utukufu na kunasibishwa na dini. Kama ambavyo kila hali ya kijamii mara nyingi inatawaliwa na vituo vya wenye nguvu, ambavyo hujikuta vinajikita katika kulinda na kuhifadhi maslahi yake dhidi ya jaribio lolote la mabadiliko au uboreshaji, linaloweza kudhuru udhibiti wake na mamlaka yake na kuathiri juu ya maslahi yake. Na ni hivyo hivyo Manabii hujikuta katika mapambano ya kukabiliana na hali iliyoenea na iliyozoeleka, anasema (swt):

**وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَإِلَى الرَّسُولِ قَالُوا حَسْبُنَا مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا ۚ أَوَلَوْ كَانَ آبَاؤُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ شَيْئًا وَلَا يَهْتَدُونَ**

**"Wakiambiwa njooni katika yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu na kwa Mtume, husema: Yanatutosha yale tuliyowakuta nayo babu zetu. Je hata kama baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka?" (Surat Maidah: 104).**

Na katika kukabiliana na uongozi wa kijamii uliochanganyikana na hali zake anasema (swt):

**وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِنْ نَذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ**

**"Na hatukumtuma mwonyaji yeyote kwenye mji ila walisema wapenda anasa wake: Hakika sisi tunayakataa hayo mliyotumwa nayo." (Surat Sabaa: 34).**

Pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu (swt) anachagua kwa ajili ya kazi ya utume na ujumbe anayefaa zaidi na mwenye uwezo zaidi:

**اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ**

**"Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi wa kujua mahali anapoweka ujumbe Wake." (Surat An'am: 124).**

Isipokuwa mapambano makali na vikwazo vyake mara nyingi hukwamisha harakati za daawa, na kuzuia uwezekano wa kufaulu kwake. Na kadiri kutokuendelea na ushirikina unavyokuwa umejikita zaidi katika jamii, na kadiri vituo vyenye nguvu vinapokuwa na nguvu zaidi, ndivyo kazi ya Nabii inavyokuwa ngumu na kukutana na matatizo zaidi. Na inahitajia juhudi kubwa zaidi na kujitolea kupana zaidi.

# NABII MUSA ANAOMBA MSAIDIZI:

Nabii Musa (as) alipotumwa na Mwenyezi Mungu kwa utume alikuta nafsi yake ipo mbele ya kazi kubwa na ngumu ambapo alikabiliana na mtawala dikteta, aliyedai uungu na anayemiliki nyezo za nguvu na ubabe, naye ni Firaun. Na katika upande mwingine jamii ya Bani Israil ambayo ananasibiana nayo Musa na ambayo alikuwa anakusudia kuinusuru na kuikomboa kutokana na unyonge na ukandamizwaji, ilikuwa imeshambuliwa na hali ya kutokuendelea, na ndani yake umekithiri uovu na nukta za udhaifu, na sio rahisi tena kutii. Kwa sababu hiyo Nabii Musa (as) alimwelekea Mwenyezi Mungu akaomba Kwake msaada Wake na kuongezewa msaidizi atakayemsaidia kubeba jukumu hili kubwa na zito:

وَاجْعَلْ لِي وَزِيرًا مِنْ أَهْلِي هَارُونَ أَخِي اشْدُدْ بِهِ أَزْرِي
وَأَشْرِكْهُ فِي أَمْرِي

**"Na nipe waziri katika watu wangu. Harun ndugu yangu. Niongeze nguvu zangu kwaye. Na umshirikishe katika jambo langu." (Surat Twaha: 29 – 32.).**

Shawkani amesema: "Yaani: Eee Mwenyezi Mungu niongeze nguvu kwaye, na mfanye kuwa msaidizi wangu katika jambo la ujumbe. Na *al-Azri* ni nguvu, husemwa: *Aazarahu*: Yaani amempa nguvu."[1] Na ni wazi kwamba kuamua kuchagua msaidizi katika watu wake, ni kutokana na faida ya uhusiano wa nasaba na ukaribu

[1] Shawkani: Muhammad bin Ali, katika *Fat'hul- Qadir*, Juz. 3, uk. 451, Chapa ya Asriya Swaida–Beirut, 1997.

ili kuimarisha ikhilasi na kusaidiana, kama ambavyo aliujua vizuri utimiaji wa sifa za uongozi katika shakhisiya ya ndugu yake Haruna, na hivyo hayo yakamsukuma yeye kumpendekeza kwa ajili ya nafasi hii ya ujumbe. Na Mwenyezi Mungu akakubali ombi la Nabii wake Musa (as):

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ وَجَعَلْنَا مَعَهُ أَخَاهُ هَارُونَ وَزِيرًا

**"Na hakika tulimpa Musa Kitabu na tukamuweka pamoja naye nduguye, Harun, kuwa waziri."** **(Sura Fur'qan: 35).**

# ALI ANA CHEO SAWA NA HARUN (AS):

Hakika anayesoma historia ya Waarabu kabla ya Uislamu na hali waliyokuwa wanaishi nayo ikiwa ni pamoja na ujahili na upotovu, ambapo walikuwa wametawaliwa na kasumba ya ukabila, mizozo, vita vya ndani, ibada ya masanamu na mizimu na muamala mgumu. Na mwenye kutafakari hali ya jamii ya Makka na kiburi cha Makuraishi na kujitukuza kwao kwa nasaba zao na ubinafsi wao, vile vile kukita kwa mizizi ya nguvu ya kiyahudi pembezoni mwa Madina na ulimbikizaji wao wa nguvu ya kiuchumi, hakika anayesoma hayo anafahamu ukubwa wa jukumu ambalo alilibeba Nabii Muhammad (saww) wakati alipopewa utume na Mwenyezi Mungu. Na anabaini ukubwa wa kazi yake tangu mwanzo:

إِنَّا سَنُلْقِي عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيلًا

**"Hakika tutakuteremshia kauli nzito."** **(Surat Muzammil: 5)**

Hivyo ni jambo la kawaida Mtume wa Mwenyezi Mungu kutaka msaidizi wa kumnusuru, na kumsaidia katika kufanya kazi ya daawa na jukumu la ujumbe. Pamoja na kwamba kundi la Masahaba wema lilimzunguka Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Masahaba ambao walitangulia katika Uislamu na wakajitolea katika kuutumikia na kuutetea, isipokuwa ukubwa wa jukumu la Mtume wa Mwenyezi Mungu lilikuwa linahitaji kuwepo msaidizi makhususi mwenye uwezo, ambaye yuko karibu na nafsi ya Mtume wa Mwe-

nyezi Mungu (saww), ambaye anaamiliana naye kwa uaminifu wa jumla na kufunguka kwa ukamilifu. Na mtu huyo hakuwa isipokuwa ni Ali bin Abu Talib (as), yeye ndiye yuko karibu zaidi na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwa nasaba baina ya Masahaba wote waliotangulia katika Uislamu na mwenye mshikamano naye zaidi katika uhusiano.

Inafahamika kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amekulia katika malezi ya Abu Talib tangu akiwa katika umri wa miaka nane baada ya kufariki babu yake Abdul-Mutwalib, Abu Talib na mke wake Fatma binti Asad mama wa Ali bin Abu Talib alibeba jukumu la kumlea Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Na alipozaliwa Ali (as) Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alikuwa na umri wa miaka thalathini, na alikuwa ameshamuoa Khadija binti Khuwailid, na rejea za historia zinaonyesha kwamba Mtume (saww) alimchukua Ali (as) nyumbani kwake kwa ajli ya kumwangalia na kumlea.

Tabari anapokea katika kitabu chake cha historia kutoka kwa Salamah kutoka kwa Abi Is'haq, amesema: "Mwanaume wa kwanza kumwamini Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na kuswali pamoja naye, na kusadikisha aliyokuja nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni Ali bin Abu Talib, na wakati huo alikuwa ni kijana wa miaka kumi. Na ilikuwa kati ya aliyoneemeshwa Ali bin Abu Talib na Mwenyezi Mungu ni kwamba alikuwa katika malezi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kabla ya Uislamu." Na kutoka kwa Mujahid bin Jabir Abi al-Hajaj amesema: "Ilikuwa ni katika neema za Mwenyezi Mungu kwa Ali bin Abu Talib na aliyomfanyia na kumtakia kheri, kwamba: Makuraishi walipatwa na matatizo na Abu Talib alikuwa na watoto wengi, Mtume akamwambia Abbas ami yake, na alikuwa ni mwenye nafasi katika Bani Hashim: 'Ewe Abbas hakika ndugu yako Abu Talib ana watoto wengi na watu wamepatwa na unayoyaona

miongoni mwa matatizo haya, twende tukampunguzie mzigo wa watoto, mimi nichukue mtu mmoja kati ya watoto wake na wewe uchukue mmoja kati watoto wake ili tumpunguzie mzigo.' Abbas akasema: 'Sawa.' Wakaondoka hadi kwa Abu Talib wakamwambia: 'Hakika sisi tunataka tukupunguzie mzigo wa watoto wako, hadi iondoke kwa watu hali waliyomo.' Abu Talib akawaambia: 'Kama mtaniachia Aqil basi fanyeni mtakavyo.' Mtume akamchukua Ali (as) kwake, na Abbas akamchukua Ja'far kwake, na Ali (as) hakuacha kuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hadi Mwenyezi Mungu akamtuma kuwa Nabii, basi Ali (as) akamfuata, akamwamini na akamsadikisha."[2]

Na Imam Ali (as) amezungumzia katika moja ya hotuba zake kulelewa kwake katika uangalizi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwa kusema: "Na mmeshajua nafasi yangu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwa ukuruba wa pekee na nafasi makhususi. Aliniweka katika mapaja yake na mimi ningali mdogo, alikuwa ananikumbatia katika kifua chake na ananilaza katika kitanda chake na ananigusisha mwili wake na ananinusisha jasho lake, na alikuwa ananitafunia kitu kisha ananilisha."[3] Na haiwezekani kukanusha athari ya malezi haya katika kutengeneza shakhisiya ya Ali (as) na ukaribu wake kwa shakhisiya ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), na kisha kumwandaa kwa ajili ya jukumu la usaidizi na uwaziri wenye kutegemewa katika kazi ya ujumbe wa Mwenyezi Mungu.

Mwanafikra wa Kimisri Abdul-Karim al-Khatib anasema: "Ni kweli kwamba Ali (as) alikuwa na hadhi kubwa zaidi, mwenye usuhuba mrefu zaidi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), alikuwa mikononi mwa Muhammad tangu alipozaliwa, kabla ya utume

[2] Tabariy: Muhammad bin Jarir, katika *Tarikh Tabari*, Juz. 2, uk. 57.
[3] Al-Musawi: Sharif Ridhaa, katika *Nahjul-Balaghah*, Hotuba namba 192.

na baada yake, hakuachana naye katika amani au vita na akiwepo nyumbani au akiwa safarini, bali alikuwa katika mikono ya Mtume na chini ya uangalizi wake na usimamizi wake hadi Mtume alipokwenda kwa Mola Wake Mtukufu, na wakati ilipotoka pumzi yake ya mwisho ya uhai alikuwa katika kifua cha Ali (as). Na wewe kama utaangalia wote ambao walikuwa katika uangalizi wa Nabii, kuanzia mke na watoto hutokuta yeyote kati yao aliyekuwa na usuhuba mrefu zaidi kwa Nabii, na katika kutangamana naye kama alivyokuwa Ali. Ali alisuhubiana na Nabii usuhuba wenye kuendelea zaidi ya miaka thalathini na muda huo hajaupata yeyote kati ya Waislamu."[4]

[4] Al-Khatib: Abdul- Karim katika *Aliyu bin Abitalib Baqiyatu Nubuwati wa Khatamil-Khilafa*, uk. 85 Chapa ya pili Darul-Ma'arifa – Beirut 1975.

# HADITH YA CHEO (*AL-MANZILAH*):

Kama alivyoomba Nabii Musa (as) kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amsaidie kwa msaidizi kutoka katika Ahali zake, ashirikiane naye katika kufanya kazi ya ujumbe, na akampendekeza ndugu yake Harun kwa nafasi hii kwa kujua kwake hatari ya mazingira ya tablighi yake, imepokewa katika rejea za Kiislamu kwamba Nabii Muhammad (saww) pia aliomba ombi kama hilo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na akampendekeza Ali (as) kwa ajili ya kuwa msaidizi wake.

Ananukuu Sayyid Alusiy al-Baghidadiy katika tafsiri yake yafuatayo: "Imekuja kwamba Nabii (saww) aliomba dua kama hii isipokuwa alimsimamisha Ali – Mwenyezi Mungu autukuze uso wake – nafasi ya Harun (as), kwani amepokea Ibnu Mardawaihi, al-Khatib na Ibnu Asaakir kutoka kwa Asmai binti Umais, amesema: Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) mbele ya Thubair akisema: 'Chomoza Thubair, chomoza Thubair. Eee Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba lile ambalo alikuomba ndugu yangu Musa: Ewe Mola Wangu! Nikunjulie kifua changu. Na unifanyie wepesi jambo langu. Na ulifungue fundo lilo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu kauli yangu. Na nipe waziri katika watu wangu, Ali ndugu yangu. Niongeze nguvu zangu kwaye. Na umshirikishe katika jambo langu. Ili tukutakase sana na tukukumbuke sana. Hakika Wewe unatuona."[5]

Na rejea za hadith zenye kutegemewa kwa Sunni na Shia zimepokea ile hadithi inayojulikana kama Hadithi ya Cheo (*Hadithul-Manzilah*), ambapo Nabii (saww) alimzingatia Ali kuwa ni mwenye cheo kama cha Harun kwa Musa:

---

[5] Al- Alusiy: Sayyid Mahmud, katika Ruhul-Ma'aniy Fiy Tafsril-Qur'an, Chapa ya nne Daru Ihiyaai Turathil-Arabaiy – Beirut 1985.

1. Katika *Sahihi Bukhari* Hadith namba 4416, kutoka kwa Mus'ab bin Sa'ad kutoka kwa baba yake: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) alitoka kwenda Tabuk, na akamwacha Ali, akasema: 'Je, unaniacha na watoto na wanawake?' Akasema: 'Je, huridhii kuwa cheo chako kwangu ni kama cheo cha Harun kwa Musa? Isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?"[6]

2. Na mfano wake imekuja katika *al-Mustadrak Alas-Sahihayn* hadith namba 4575, kutoka katika njia ya Bakir bin Mismaar, kutoka kwa Amir bin Sa'ad kutoka kwa baba yake Sa'ad. Na imekuja humo kwa njia nyingine katika hadithi namba 3294.[7]

3. Na ameipokea Muslim katika *Sahih* yake hadith namba 2404 kwa njia tatu: Kutoka kwa Said bin Musayab kutoka kwa Amir bin Sa'ad kutoka kwa baba yake Sa'ad, na kutoka kwa al-Hakam, kutoka kwa Mus'ab bin Sa'ad kutoka kwa baba yake, na kutoka kwa Bakir bin Mismaar, kutoka kwa Amir bin Sa'ad kutoka kwa baba yake Sa'ad.[8]

4. Na katika *Musnad Ahmad bin Hanbal* imekuja kwa njia nyingi, kama vile Hadith namba 14693 kwa njia ya Jabir bin Abdillahi. Na hadith namba 3062 kutoka kwa Ibn Abbas. Na hadith namba 1490, na namba 1509, na namba 1505, na namba 1583, na namba 1600, kutoka kwa Sa'ad bin Abi Waqas.[9]

5. Na ameipokea Ibnu Maajah katika *Sunan* yake katika mlango wa Fadhila za Ali, kutoka kwa Ibnu Saabit naye ni Abdurahman, kutoka kwa Sa'ad bin Abi Waqas amesema: "Muawiya al-

[6] Al-Bukhariy: Muhammad bin Ismail katika Sahih Bukhariy, Hadith namba 4416.

[7] Al-Hakim Nisaburiy: Muhammad bin Abdillahi, katika Mustadrak Alas-Sahihayn, Hadith namba 4575 na Hadith namba 3294.

[8] Al- Qushairy: Muslim bin al-Hajaj, katika Sahihi Muslim, Hadith namba 2404.

[9] Ibnu Hanbali: Imam Ahmad, Musnad Imam Hanbal, Chapa ya kwanza, Alamul-Kutubi – Beirut 1998.

iporudi kutoka katika moja ya safari zake, Saad aliingia kwake na wakamtaja Ali (as), Muawiya akamshutumu Ali, ndipo Saad akakasirika na akasema: 'Unasema haya kwa mtu ambaye nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: 'Yeyote ambaye mimi ni mtawala wake basi Ali ni mtawala wake.' Na nilimsikia akisema: 'Wewe kwangu mimi una cheo sawa na cha Harun kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu.' Na nilimsikia akisema: 'Nitamkabidhi bendera kesho mtu ambaye Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanampenda.''[10]

Na mwenye kufuatilia sanad za hadith na njia za mapokezi yake itambainikia kwamba imepokewa na kundi kubwa kati ya Masahaba kama vile Jabir bin Abdillahi al-Answariy, Abi Said al-Khudriy, Abdillahi bin Abbas, Abdillahi bin Mas'ud, Anas bin Malik, Zaid bin Arqam, Abi Ayub al-Answariy, Asmai binti Umays, Ummu Salama na wengineo. Kama ambavyo imepokewa kwa matamko mengi na katika sehemu zaidi ya moja na minasaba mbalimbali miongoni mwayo ni vita vya Tabuk, nayo haiishii hapo tu, bali imepokewa pia katika sehemu zingine vilevile.

Na mbali na majadiliano ya kimakundi na kimadhehebu hakika hadith ni sahihi katika sanad, ni riwaya thabiti na imeafikiwa baina ya Waislamu, nayo inaonyesha kwamba Ali (as) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ana cheo kama cha Harun kwa Musa ukiondoa utume ambao alikuwa nao Harun, na hakuna utume baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Ikiwa Harun anamfuatia Musa katika cheo na fadhila na alikuwa mshirika wake, msaidizi wake na tegemeo lake katika kubeba jukumu la daawa na ujumbe, hakika cheo hiki kimethibiti kwa Ali bin Abu Talib kwa maelezo ya nususi na hadithi.

[10] Ibnu Majah al- Qazuwiniy: Muhammad bin Yazid, katika *Sunan Ibnu Majah*, katika Fadhila za Ali.

# MALEZI NA MAANDALIZI

Hakika somo muhimu ambalo ni wajibu tufaidike nalo katika yaliyotangulia ukiongezea na kujua cheo cha Ali na nafasi yake yenye kufahamika, ni nafasi ya malezi na maandalizi katika kutengeneza shakhsiya yenye uwezo. Alishataka Mwenyezi Mungu Ali bin Abu Talib kuchukua nafasi ya juu katika kutumikia ujumbe wa Mwenyezi Mungu, akamwandalia mazingira maalum ya malezi, ambapo amelelewa katika uangalizi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) tangu utotoni mwake, na ameleleka katika mikono yake tangu umri wake wa mwanzo, na hivyo alikuwa mbali na athari za mazingira ya ujahilia na shirki, yeye hakusujudia sanamu kamwe, na kwa sababu hiyo Waislamu wamemfanya ni mahususi bila ya Masahaba wengine kwa kauli ya: “Karamallahu Wajihahu” (Mwenyezi Mungu ameutukuza uso wake), kama ambavyo shakhsiya ya Mtume (saww), tabia njema, kigezo chema na mwalimu bora, sifa hizi zimemwangazia Ali (as) njia ya maisha ya ujumbe na jihadi.

Hakika sisi kama tunataka na tunatamani kutengeneza vizazi vyetu na watoto wetu basi ni juu yetu tuwaandalie mazingira ya malezi mema, na hiyo ni kwa sisi wenyewe kushikamana kwanza na njia ya wema na msimamo, kwani familia bora ndio inayoweza kulea mtoto mwema. Hakika mwanadamu kubeba jukumu la watoto wake na familia yake, ni wajibu kuwe kunamsukuma katika kushikamana na misingi ya dini na hukumu zake, tabia njema na sifa njema. Hayo ndio yanayomuwezesha kufanya kazi yake ya malezi, na nafasi yake ya kuelekeza, hakika baadhi ya wazazi wanakuwa dhaifu mbele ya misukumo ya raghaba na matamanio na wanaruhusu katika nafsi zao kufanya baadhi ya mambo yaliyoharamishwa, lakini mbali na mitazamo ya familia zao na watoto wao, wakati ambapo wao wa-

nawaelekeza watoto wao kuwa wema wenye kushikamana na dini. Je wanatarajia kwa maneno yao matupu wataacha athari katika nafsi za watoto wao? Hakika maelekezo sahihi ambayo yanaafikiana na mwenendo ulionyooka na mwema, ndio maelekezo yenye kuathiri. Anasema Imam Ali (as) juu ya malezi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) kwake: "Na nilikuwa namfuata kama mtoto anavyofuata nyayo za mama yake, ananifundisha kila siku elimu kupitia tabia yake njema, na ananiamrisha kuifuata."

# MFUMO WA USAWA

Mwanadamu alikabiliwa sana na bado angali anakabiliwa na siasa ya mfarakano na ubaguzi baina ya watu, kwa msingi wa ubaguzi wa ukabila au makundi ya kidini au uchumi wa kitabaka. Ambapo kuna kundi linaitakidi juu ya ubora wake kwa wengine na linajitofautisha kwao kwa ubora, na linaamiliana nao kwa kuwazingatia kuwa wao ni binadamu au raia wa daraja la chini. Na neno ubaguzi linaelezea kitendo cha kumnyima mtu au kundi fulani usawa katika nafasi, haki na wajibu.

Katika upande wa kielimu haujathibiti usahihi wa nadharia yoyote ya ubaguzi, ambayo inadai baadhi ya vizazi na koo za kibinadamu zina uwezo kuliko nyingine, na nyingine hazina uwezo kushinda nyingine. Asili ya ubinadamu ni moja katika koo zote na vizazi, utayari na uwezo unashabihiana, pamoja na kwamba jamii na mazingira yana nafasi katika kukuza vipaji na kuibua uwezo, hivyo zinaweza kurundikana sababu za kihistoria na kijamii zenye kukwamisha mazingira ya mwamko na maendeleo katika baadhi ya Ummah na mataifa, wakati ambapo cheche za mwamko zinawaka katika Ummah zingine na mataifa mengine, kwa ajili ya sababu na vyanzo vya kimaudhui, vinavyojadiliwa na utafiti wa falsafa ya historia na utamaduni. Na kitendo cha kuchomoza vipaji vya kipekee na mahiri katika koo na jamii mbalimbali kinatosha kuwa ni dalili ya kuanguka madai ya nadharia za ubaguzi. Kama inavyoshuhudia historia ya binadamu, mpishano na mfuatano wa maendeleo ya ustaarabu baina ya Ummah mbalimbali katika ardhi, hakuna ukoo au kizazi kinachomiliki peke yake msafara wa maendeleo katika historia.

Na Maulamaa wamezungumzia suala la ubaguzi na kile kinachoitwa kupevuka kwa ubaguzi au ukabila, na wamejaza utafiti na

uchambuzi, na hatimaye ikabainika kwao upuuzi wa madai yanayosema kuwepo kwa tofauti za kiukabila za kiasili baina ya binadamu. Na ili kufafanua hilo jopo la maulamaa na wabobezi katika elimu ya kurithiana na elimu ya viumbe kwa ujumla (baiologia), elimu ya ya jamii, elimu ya antoplojia (elimu ya binadamu) walikutana katika makao ya Unesco Ufaransa na wakatoa ripoti ya mwaka, humo wanaeleza ubatilifu wa nadharia ya ubaguzi.[11] Kama ambavyo uhusiano wa kidini hausihi kuwa kisingizio cha siasa ya mfarakano na ubaguzi, hakuna dini sahihi inayoshajiisha wafuasi wake juu ya ubaguzi na dhulma, Mwenyezi Mungu Mtukufu amewatuma Manabii wake na ameteremsha sharia ili kueneza uadilifu na kheri baina ya watu, anasema (swt):

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ
لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ ۖ وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ
وَمَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ ۚ إِنَّ
اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ

**"Kwa hakika tuliwatuma Mitume Wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na mizani, ili watu wasimamie uadilifu, na tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu, na ili Mwenyezi Mungu amjue anayemnusuru Yeye na Mitume Wake kwa ghaibu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda." (Surat Hadid: 25)**.

Na anasema (swt):

---

[11] Al-Kayaliy: Abdul-Wahab katika Mausu'atu Siyasiyah, Juz. 4, uk. 250, Chapa ya Kwanza 1986, Muasasatu al-Arabiyati Lilidiraasati Wanashiri - Beirut.

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ ۚ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

**"Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na hisani na kuwapa jamaa na anakataza uchafu na uovu na dhulma. Anawapa mawaidha ili mpate kukumbuka." (Surat Nahli: 90)**.

Na kundi lolote linalofanya ubaguzi baina ya watu, na linalingania wafuasi wake kutotambua haki za wengine kwa jina la dini, ni lazima litakuwa limekosea katika kuifahamu dini au limekusudia kuitumia vibaya. Kwa hili linabainika kosa la yale ambayo yanategemewa na siasa ya ubaguzi kwa kisingizio cha nadharia. Na katika upande wa tabia njema, hakika kufanya ubaguzi baina ya watu katika yale ambayo ni wajibu kuwe na usawa baina yao, kunazingatiwa kuwa ni kuvunja Haki za Binadamu, na ni uadui katika heshima yake, na ni uovu na dhulma dhidi ya anayefanyiwa siasa hii. Tangazo la ulimwengu la Haki za Binadamu katika ibara yake ya kwanza limetamka yafuatayo:

"Watu wote wanazaliwa wakiwa huru wako sawa katika heshima na haki, na wamepewa akili na dhamira, na ni wajibu kuamiliana wao kwa wao kwa roho ya udugu."

Na ibara ya pili inasema:

"Kila mwanadamu ana haki ya kufurahia kila haki na uhuru uliotajwa katika tangazo hili bila ya ubaguzi wowote, kama vile ubaguzi unaosababishwa na kasumba au rangi au jinsia au lugha au dini au rai ya kisiasa au rai nyingine yoyote au asili ya uraia au kijamii au pato au uzawa au hali nyingine yoyote."

# UBAGUZI, HATARI NA MADHARA:

Ama katika kiwango cha matokeo ya kivitendo, hakika siasa ya ubaguzi inasababisha madhara makubwa na hatari kubwa, na kati ya madhara yanayoonekana zaidi ni haya yafuatayo:

**Kwanza:** Kudhoofisha umoja wa kijamii, hivyo hautapatikana mshikamano abadani baina ya makundi ya jamii ambayo baadhi wanajikweza juu ya wengine, wana upendeleo katika ubora na kipato. Na umoja na mshikamano unaoonekana huwa ni hali ya uongo na udanganyifu, haukawii kuzimika na kupotea wakati wa mtihani.

**Pili:** Kutishia amani na utulivu. Wale wenye kudhurika kutokana na ubaguzi humea katika nafsi zao na ndani yao ghadhabu inayowasukuma kulipiza kisasi na kutetea heshima yao na kuondoa uadui dhidi ya haki zao. Na katika mazingira haya ya ubaguzi wenye kupindukia, yanaweza kujitokeza makundi yenye kupingana nje ya utawala na udhibiti, jambo ambalo huiingiza jamii katika mzozo wa kulipiza kisasi, na kusababisha hali ya khofu na mkanganyiko.

**Tatu:** Kunufaika kwa watu wa nje. Kila Ummah na jamii ina maadui na washindani wa nje, wanajali kunufaika na hali ya ndani, na kupenya kupitia mianya na nukta za udhaifu, hivyo kuwepo kundi katika jamii linalohisi unyonge na kupunjwa haki, kunawapa maadui wa nje fursa bora, hususan katika zama hizi ambazo dola kubwa zinanufaika na nembo ya Haki za Binadamu, na madai ya kutetea walio wachache.

**Nne:** Kuuwa nguvu na kupuuza vipaji, na kuleta udhaifu katika kunufaika kutokana na uwezo wa wanajamii, maadamu kipimo ni uhusiano wa kikabila au kidini au kitabaka na sio uwezo na ikhilasi.

# BAINA YA YALIYOPITA NA YALIYOPO:

Sheria ya Kirumi ilikuwa inawagawa watu kati ya walio huru na wasio huru, na hawa walio huru pia walikuwa matabaka mawili: Walio huru kwa asili nao ni Warumi, na wasio wa asili, nao ni Walatini. Ama wasiokuwa huru walikuwa aina nne: Watumwa, walioachwa huru, walio huru nusu, na watumwa wanaofuata ardhi. Na walio huru kwa asili peke yao walikuwa wanapata haki za kisiasa katika wakati mwingi ambao historia ya Roma imeupitia, ama wasiokuwa wao walikuwa wananyimwa hayo.

Na jamii ya Kiirani katika zama za Sasaniya ilikuwa imeasisiwa katika mazingatio ya nasaba na kazi, na baina ya matabaka ya jamii kulikuwa na pengo kubwa ambalo halizibiki kwa daraja wala haliunganishwi na kiunganishi chochote, na serikali ilikuwa inaharamisha mtu yeyote wa kawaida kati yao kununua ardhi ya kiongozi au mkuu. Na ilikuwa katika kanuni za siasa ya Sasaniya ni kila mmoja kukinaika kwa nafasi yake ambayo amepewa na nasaba yake na wala asiangalie yaliyo juu yake, na haikuwa ni haki kwa yeyote kufanya kazi isipokuwa kazi ambayo Mwenyezi Mungu amemuumbia. Na kabla ya kuzaliwa Isa (as) kwa karne tatu, ulistawi utamaduni wa Barahamiya huko India, ambao waliweka kanuni inayojulikana kwa Montashaster, inayowagawa wananchi katika matabaka manne nayo ni: Barahima, nao ni makuhani na watu wa dini. Na tabaka la Shatariy, nao ni wapiganaji. Na tabaka la Waish, nao ni wakulima na wafanyabiashara. Na tabaka la Shaudar, nao ni watumishi wa matabaka haya matatu.

Na kanuni hii imelipa ubora na haki tabaka la Barahima na kuwafanya ni waungu, na tabaka la nne Shaudar lilikuwa linawakilisha waliodharauliwa ambao hawana thamani au haki yoyote. Na katika mwaka 1948 serikali ya India ilianza kupiga vita mgawanyo huu wa kitabaka, pamoja na kwamba kumetokea baadhi ya maendeleo isipokuwa athari na mabaki ya hali hii bado ingali ipo katika sehemu nyingi za India.

Na Waafrika huko Marekani wamekabiliwa na ubaguzi mkubwa, katika kipindi ambacho ni kabla ya karne ya kumi na tisa. Na tangu mwanzo wa karne ya kumi na tisa kumekuwa na kanuni katika sehemu mbalimbali za Marekani zenye kuunga mkono utengano na ubaguzi baina ya weupe na weusi, kwa kila kundi kati yao kutumia sehemu za huduma kwa Ummah kwa kujitenga. Kwa mfano, jimbo la Oklahoma limelazimisha kwa weusi na weupe kutumia vioski vya simu kwa kila kundi vioski vyao, kama ambavyo jimbo la Arkansas limetenganisha meza za kuchezea kamari baina ya meza ya weusi na weupe. Wakati ambapo mahakama zilitumia Injili tofauti kati ya ile anayotumia mweupe na ile anayotumia mweusi kwa ajili ya kuapa wakati wa kutoa ushahidi, kama ambavyo majimbo ya Kusini yametunga kanuni ambazo zimewatoa weusi katika haki zao za uchaguzi.

Na hali ya ubaguzi na utengano imeendelea muda wote wa karne ya kumi na tisa takriban, kisha ikaanza kupungua na kumalizika pole pole katika muongo wa pili wa karne ya ishirini. Na katika mwaka 1969 Mahakama Kuu ya Marekani ililazimisha shule za Ummah katika sehemu mbalimbali, kuzuia mara moja siasa ya utengano wa kijamii. Na hata katika miaka ya themanini, weusi walikabiliwa na kutengwa kijamii katika sehemu za makazi. Na licha ya kutolewa kanuni nyingi ambazo zinazuia ubaguzi na utengano wa kibaguzi huko Marekani, lakini bado hali inavuka kanuni katika maeneo na misimamo mingi, ambapo bado watu weusi wangali wanaishi ka-

tika kiwango cha chini kuliko weupe, katika nyanja ya uchumi na kijamii.

Na Ulaya ubaguzi wa kidini ulikuwepo kwa karne nyingi, kuanzia karne ya tano hadi karne ya kumi na sita. Ulielekezwa kwa sifa ya msingi dhidi ya Wayahudi wa Ulaya, ambapo ilikuwa ni juu yao katika nchi nyingi isipokuwa Hispania, ambapo ilikuwa katika kivuli cha ustaarabu wa Kiislamu, ilikuwa ni juu yao kuishi ndani ya vitongoji vya wachache vya Wayahudi vinavyojulikana kwa jina la Ghetto. Kama ambavyo kanuni ziliwazuia kumiliki ardhi, na kujiunga na vyama vya wafanyakazi au kutumia tiba au kanuni, jambo ambalo lilisababisha washindwe kupata kazi, isipokuwa zile kazi ambazo wanazikwepa Wakristo.

Na serikali ya watu weupe huko Afrika Kusini ilifuata mfumo mbaya wa siasa ya ubaguzi katika zama hizi, ambapo ilikusanya siasa ya utawala kwa weupe wachache ambao kwa asili wanatoka Ulaya, miongoni mwa wajukuu wa wakazi wa Uholanzi wa awali ambao wanajulikana kwa jina la Waafrikana, na wao wana idadi ya asilimia 14 kati ya wakazi wote, na walitumia siasa ya ubaguzi na utengano wa kibaguzi dhidi ya wakazi wengi walio weusi, ubaguzi ambao ulitangazwa na chama cha ukabila kilipofika madarakani mwaka 1948, na kiliwatengea weusi sehemu maalum kwa ajili ya maisha yao isiyozidi asilimia 13 ya eneo la nchi nzima, na ilikuwa ni juu yao kuonyesha vitambulisho vyao wakati wa kuingia katika sehemu wanayoishi weupe. Shule za serikali zilikuwa zimetenganishwa kwa ubaguzi, kama ambavyo haikuwa inawezekana kwa wasio weupe kupata kazi bora zilizotengwa kwa ajili ya weupe, na siasa hii iliendelea hadi mwaka 1991 ambapo ilifutwa kutokana na msimamo na mapambano ya wananchi wakiungana pamoja na mataifa mengine.

Imebakia Israil kuwa ni ngome kubwa ya vitendo vya kibaguzi vya kidhalimu, yenye kulindwa na kuhifadhiwa kwa msaada

wa Marekani, inafukuza na kuhamisha wananchi wa Palestina na watu wake wa kisharia na kuleta Wayahudi wageni kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu, ili waishi katika ardhi za Palestina na kuwafanyia kila aina za dhulma na ujeuri wenyeji. Na katika nchi nyingi za ulimwengu kuna hali za ubaguzi baina ya watu, waziwazi au kwa kisiri, unafanyika kwa muundo, aina na madai mbalimbali.

# UISLAMU NI SHARIA YA USAWA

Kabla ya karne kumi na nne, wakati watu walipokuwa wanakandamizwa chini ya ukandamizaji wa siasa ya ubaguzi kwa anwani mbalimbali, Uislamu ulikuja na kufungua zama mpya ya ubinadamu, humo ananeemeka mwanadamu kwa usawa ambao unadhamini kwake heshima yake na haki yake ya ubinadamu. Qur'ani Tukufu imetamka juu ya umoja wa asili ya binadamu, kutofautiana kwa koo, utaifa, dini, ukabila ni ndani ya duara hili moja la ushirikiano, nayo ni tofauti inayotakiwa na hekima ya Mwenyezi Mungu ili kuboresha maisha ya binadamu, na kukamilisha mwendeo wake. Anasema (swt):

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا ۚ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ

**"Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumewafanya mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mtukufu zaidi yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye na takua zaidi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye habari." (Surat Hujurat: 13).**

Hakika ni wito unaoelekezwa kwa watu wote, na neno *An-Naas* (Watu) ni istilahi inayoelezea juu ya jinsia ya kibinadamu, nayo ni istilahi haikubali mgawanyo na utengano, kama vile istilahi ya *Ummah* (Ummah) ambayo inamaanisha kundi la watu na wingi wake ni *umam*. Na vile vile Sha'ab (Taifa) na wingi wake ni *Shu'ub* (Mataifa), na vile vile *Mujtama'a* (Jamii) na wingi wake ni *Mujtamaati*

(Jamii). Ama *An-Naas* (Watu) linajumuisha binadamu wote, na kwa hiyo hakuna nafasi ya mgawanyo isipokuwa katika njia ya kuongeza, na ni tamko lisilo na wingi.

Mtume Muhammad (saww) ametilia mkazo msingi wa usawa katika hadithi na misimamo mingi, kama vile kauli yake (saww): "Watu wako sawa kama vile meno ya kitana."[12] Na amesema (saww) katika hotuba yake katika Hija ya kuaga: "Enyi watu! Hakika Mola wenu ni Mmoja na hakika baba yenu ni mmoja, nyote mwatokana na Adam na Adam anatokana na udongo, hakika aliye mbora kati yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule aliye mchamungu kuliko wote. Mwarabu hana ubora wowote juu ya asiyekuwa mwarabu, wala mweusi juu ya mwekundu na wala mwekundu juu ya mweusi isipokuwa kwa uchamungu, bila shaka nimefikisha." Wakasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) amefikisha. Akasema: "Aliyepo amfikishiye asiyekuwepo, kwani huenda mfikishiwaji ni mwenye kufahamu kuliko msikilizaji."[13]

Na Dkt. Twaha Husain anaona kwamba "Uislamu umekuja kabla ya kila kitu katika mambo mawili: La kwanza ni Tawhid na la pili ni usawa baina ya watu. Na lililowakasirisha zaidi Makuraishi kati ya yale yaliyowakasirisha kutoka kwa Nabii na daawa yake ni kwamba alikuwa analingania kwenye usawa, na hakuwa anatofautisha baina ya bwana na mtumwa, na wala baina ya muungwana na mtwana, wala baina ya mwenye nguvu na mnyonge, baina ya tajiri na fakiri, bali alikuwa analingania watu wote wawe sawa kama meno ya kitana wasijibague na kubaguana wao kwa wao, wala baadhi wasijikweze juu ya wengine."[14]

---

[12] Sarkhisiy: Shamsu Diyn, katika *al-Mabusut*, Juz. 5, uk. 23, Darul-Maarif- Beirut, 1406 Hijiria.

[13] Swaalihiy Shaamiy: Muhammad bin Yusuf, katika *Subulul-Hudaa Warashaadiy Fiy Sirati Khairil-Ibaad*, Juz. 8, Uk. 482, Chapa ya kwanza 1993, Darul-Kutubil-Ilimiya – Beirut.

[14] Husain: Dkt. Twaha, katika *Fitinatul- Kubraa*, Juz. 1, uk. 10.

# MFUMO WA USAWA:

Sira ya Imam Ali (as) katika utawala pamoja na ufupi wa umri wake, inatengeneza mfano bora wa utekelezaji wa sharia ya usawa katika Uislamu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Imam Ali (as) alishika hatamu za ukhalifa na utawala kwa kupewa kiapo cha utii na watu wote, baada ya kipindi cha fitina na mkanganyiko uliopelekea kuuliwa Khalifa wa tatu Uthman bin Affan, na wakati huo ilikuwa imeshadhihiri katika jamii ya Kiislam hali na mazingira mapya, kwa sababu ya kupanuka ramani ya nchi za Kiislamu na kuingia jamii zingine katika duara la dola ya Kiislamu, na hatimaye pato la Baitul-Mali likawa kubwa, na kulikuwa na siasa ambayo ilifuatwa katika kugawa mapato ya mali na hivyo kujitokeza tamaa za kisiasa na uroho wa kimaslahi.

Imam Ali (as) alitangaza tangu siku ya kwanza ya ukhalifa wake kushikamana kwake na mfumo wa usawa baina ya Ummah na raia wa dola ya Kiislamu, na akatilia mkazo hilo kupitia siasa yake ya kivitendo na misimamo yake na maelezo yake mengi, kama vile waraka wake kwenda kwa Maliki al-Ashtar alipompa ugavana wa Misri, nchi yenye dini mbalimbali, kwa vile baadhi ya watu wake walikuwa wamebakia katika Ukristo. Miongoni mwa vipengele vya barua hiyo ni kauli yake (as):

وَأَشْعِرْ قَلْبَكَ الرَّحْمَةَ لِلرَّعِيَّةِ، وَالْمَحَبَّةَ لَهُمْ، وَاللُّطْفَ بِهِمْ، وَلاَ تَكُونَنَّ عَلَيْهِمْ سَبُعاً ضَارِياً تَغْتَنِمُ أَكْلَهُمْ، فَإِنَّهُمْ صِنْفَانِ: إِمَّا أَخٌ لَكَ فِي الدِّينِ، وَإمّا نَظِيرٌ لَكَ فِي الْخَلْقِ،

**"Uzoeshe moyo wako kuwa na huruma kwa raia, na upendo kwao, na kuwatendea wema. Na wala usiwe mnyama mkali mwenye madhara kwao, ukavizia fursa ya kuwang'ata (kuwatafuna), kwani wao (raia) wako wa aina mbili: Ama ni ndugu yako katika Dini au ni mfano wako katika kuumbwa (ni binadamu kama wewe)."[15]**

[15] Al-Musawiy: Sharifu Ridhaa, katika *Nahjul-Balaghah*, Barua ya 53.

# USAWA KATIKA KUTOA:

Mapato ya Baitul-Mali miongoni mwa Zaka, kodi na ngawira, yalikuwa yanatumika katika maslahi ya dola ya Kiislamu, na yanayobaki yanagawiwa kwa Ummah. Katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) na zama za Khalifa wa kwanza Abu Bakr na sehemu ya zama za ukhalifa wa pili Umar, pato lilikuwa linagawiwa kwa usawa baina ya Waislamu, na katika mwaka wa ishirini Hijiria Khalifa Umar alivumbua mpango mpya wa kuendesha Baitul-Mali na akaona kuwepo na mpango wa upendeleo katika kutoa, ili kuwadhihirisha waliotangulia katika historia ya jihadi.

Imekuja katika *Twabaqatul-Kubra* cha Ibn Sa'ad: "Umar bin al-Khatab alipoamua kuandika orodha, na hiyo ni Muharram mwaka wa ishirini, alianza na Bani Hashim katika daawa, kisha waliokaribu zaidi na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), Umar akaweka ubora kwa walio katika orodha, ubora ukawa kwa waliotangulia, akawapendelea katika mgao wale waliotangulia. Abu Bakr as-Swidiq alikuwa ameweka usawa baina ya watu katika mgao, Umar akaambiwa hilo, lakini yeye akasema:

'Sitomfanya aliyempiga vita Mtume sawa na aliyepigana pamoja naye.' Akaanza na waliohudhuria Badri miongoni mwa Muhajirina na Answar, akaweka kwa kila mtu miongoni mwao dirham 5000 kwa kila mwaka, na washirika wao na huria wao wakawa sawa pamoja nao. Na akaweka kwa wale ambao wana Uislamu kama Uislamu wa watu wa Badri miongoni mwa Muhajirina wa Uhabeshi, na waliohudhuria Uhud, dirham 4000 kila mtu miongoni mwao. Na akaweka kwa watoto wa watu wa Badri dirham 2000 isipokuwa Hasan na Husain (as), hakika wao aliwaunganisha na fungu la baba yao kwa ukaribu wao na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Akaweka kwa aliyehama kabla ya Ukombozi wa Makka kwa kila mtu mion-

goni mwao dirham 3000. Na akaweka kwa kila Mwislamu mwanamke wa Ukombozi wa Makka, kila mtu miongoni mwao dirham 2000. Na akaweka kwa vijana wadogo miongoni mwa watoto wa Muhajirina na Answar, fungu la Mwislamu mwanamke wa Ukombozi wa Makka. Kisha akaweka kwa watu kulingana na vyeo vyao na usomaji wao wa Qur'ani na jihadi yao. Kisha akaweka kwa watu waliobakia mlango mmoja, akawaunganisha waliokuja baada yao miongoni mwa Waislamu wa Madina dinar ishirini na tano kwa kila mtu, na akaweka kwa waliokombolewa pamoja nao, na akaweka kwa watu wa Yemen na sehemu ya Sham na Iraki kila mtu dirham 2000, elfu moja, mia tisa, mia tano hadi mia tatu, hakumpa yeyote chini ya mia tatu."[16]

Siasa hii baadaye ilileta athari mbaya aliyoiona Umar, na akaazimia kurudi nyuma lakini kifo hakikumpa nafasi, imepokewa kutoka kwa Zaid bin Aslam kutoka kwa baba yake amesema: "Nilimsikia Umar bin al-Khattab anasema: 'Naapa kama nitabaki hadi mwaka ujao, nitamuunganisha mtu wa mwisho na wa kwanza wao, na nitawafanya kuwa ni mtu mmoja tu.'" Na katika nukuu nyingine: "Kama nitabakia hadi mwakani nitamuunganisha wa chini wao na wa juu wao."[17]

Na siasa ya ubaguzi katika kutoa iliendelea baada ya hapo kwa muda wote wa Khalifa Uthman na ikazidi makali ya athari zake mbaya, kwa vitendo vya baadhi ya wasaidizi wa Khalifa na jamaa zake wa karibu, jambo ambalo liliimarisha hali ya matabaka na kuimarisha hali ya ubaguzi baina ya watu, na ikaleta kisasi na ghadhabu kwa watu wengi katika jamii. Kwa sababu hiyo Imam Ali (as) aliazimia kutatua tatizo hili tangu siku ya kwanza ya ukhalifa wake, na akalifanya kuwa ni msingi wa vipaumbele vyake. Akachukua maamuzi

[16] Ibnu Sa'ad, katika *Twabaqaatul-Kubra*, Juz. 3, Uk. 296 – 297 Daru Swadir – Beirut 1957.

[17] Rejea iliyotangulia Uk. 302.

yake makali kwa kufuta siasa ya ubaguzi katika kutoa na akafanya usawa baina ya watu bila ya upendeleo au ubaguzi wowote.

Hakika ni lazima nguvu na pande hizo zilizokuwa zinazonufaika na siasa ya awali zikasirishwe, lakini yeye alikabiliana na hilo kwa umadhubuti na ushujaa, kwa kuiandaa nafsi yake kwa kuvumilia hatari za ziada ambazo zinaweza kukumba utulivu wa utawala na uongozi wake, kwa kuitakidi kwake kwamba usawa ni msingi ambao haukubali suluhu juu yake, na hakuna kutanazali juu yake, hata kama thamani ya hilo ni kutetereka utawala, kwa sababu utawala kwake haukuwa ni kusudio na lengo, bali ni wasila tu wa kutekeleza misingi na malengo ya Kiislamu. Imam alielekeza ueleweshaji wa kiutamaduni na maarifa kwa watu wa Ummah ili kuweka wazi mfumo wake na siasa yake.

Amepokea Ibnu Abil-Hadid katika *Sharhu Nahjul-Balaghah*, kutoka kwa Sheikh wake Abi Ja'far al-Iskaafiy, kwamba Ali (as) alipanda mimbari siku ya pili ya kupewa kwake kiapo cha utii, nayo ni siku ya Jumamosi ikiwa zimebakia siku kumi na moja za mwezi wa Dhulhija, na hotuba yake ilikuwa:

**"Eee wasije watu miongoni mwenu wakasema kesho, dunia iliwatawala hivyo wakatumia ardhi, wakapasua chemchem, wakapanda farasi na wakachukua watumishi na mahema, na hatimaye hilo likawa ni aibu na fedheha kwao. Ninapowakataza wao yale ambayo walikuwa wanajiingiza humo, na nikiwapa haki zao wanazozijua wanachukia hayo na wanakataa na wanasema: 'Mtoto wa Abu Talib ametunyima haki zetu.' Eee mtu yeyote kati ya Muhajirina na Answari katika Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kama anaona kwamba ana ubora kuliko mwingine kwa usahaba wake, hakika ajue ubora ni nuru kesho mbele ya Mwenyezi Mungu, na thawabu yake na malipo yake ni kwa Mwenyezi Mungu. Na mtu yeyote anayemwitikia Mwenyezi Mungu na Mtume, amesadikisha mila yetu na ameingia katika dini yetu na ameelekea kibla chetu. Bila shaka**

**atakuwa amewajibika kupata haki za Uislamu na mipaka yake. Nyinyi ni waja wa Mwenyezi Mungu, na mali ni mali ya Mwenyezi Mungu, inagawanywa baina yenu kwa usawa, hakuna ubora humo kwa yeyote na wachamungu wanayo malipo mema mbele ya Mwenyezi Mungu na thawabu bora zaidi. Mwenyezi Mungu hakuijalia dunia kuwa ni malipo wala thawabu kwa wachamungu, na yaliyopo kwa Mwenyezi Mungu ni bora kwa watu wema.”**

Sahli bin Hunayf akasema: “Ewe Amirul-Muuminina, huyu alikuwa mtumwa wangu jana na leo nimemwacha huru.” Akasema: “Tutampa kama tunavyokupa.” Akampa kila mmoja kati yao dinari tatu na hakumpendelea yeyote.[18] Na katika kujibu madai ya kustahiki upendeleo kwa kutangulia katika Uislam na jihadi amesema (as) katika moja ya hotuba zake:

**“Enyi Muhajirina na Answaar! Mnajivunia kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake Uislamu wenu, bali Mwenyezi Mungu ana fadhila kwenu kwa kuwaongoa katika imani kama nyinyi ni wa kweli. Ama katika mali hii hakuna mtu yeyote mwenye ubora kushinda mwingine, na Mwenyezi Mungu ameshamaliza mgao wake. Ni mali ya Mwenyezi Mungu na nyinyi ni waja wa Mwenyezi Mungu Waislamu, na hiki ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu tumekikubali na tumejisalimisha kwake, na ni ahadi ya Nabii wetu iliyopo baina yetu, hivyo yeyote ambaye hajaridhika nacho basi afanye atakavyo, hakika mwenye kufanya kwa kumtii Mwenyezi Mungu, na mwenye kuhukumu kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu, hana khofu juu yake.”**[19]

Na kati ya mambo yaliyomkasirisha Twalha na Zubair ilikuwa ni kitendo cha Ali (as) kufuata mfumo huu na kufuta upendeleo wao katika mgao, na walimweleza hilo wazi bayana, na yeye akawajibu kwa ukali: “Ama kauli yenu: ‘Umejaalia fungu letu na fungu la

[18] Ibnu Abil-Hadid: Abdul- Hamid katika *Sharhu Nahjul-Balaghah*, Juz. 7, uk. 37, Chapa ya kwanza 1987 Darul-Jalil - Beirut.

[19] Rejea iliyotangulia uk. 40.

panga zetu na mikuki yetu, sawa na fungu la wasiokuwa sisi.' Jueni zamani walitangulia katika Uislamu watu ambao waliunusuru kwa panga zao na mikuki yao, na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) hakuwapendelea katika mgao wala hakuwapendelea kwa kutangulia kwao, na Mwenyezi Mungu (swt) atamlipa aliyetangulia na mpigana jihadi Siku ya Kiyama kwa amali zao, na Wallahi hamna nyinyi wala asiyekuwa nyinyi kwangu mimi fungu lolote isipokuwa hili."[20]

Na Imam Ali (as) alimpa uongozi wa Baitul-Mali ya Madina Ammaar bin Yaasir na Abu Haytham bin at-Tihaani, akaandika (as): "Mwarabu, Mkuraishi, Answaar, asiyekuwa mwarabu na kila aliyeko katika Uislamu miongoni mwa makabila ya kiarabu na wasiokuwa Warabu wako sawa."[21] Na kuna kundi miongoni mwa Shia wa Ali na wafuasi wake lilikuja likihofia utawala wa Ali kutokana na upinzani wa sehemu zenye nguvu, wakasema: "Ewe Amirul-Muuminina, lau ungetoa hizi mali na kuwagawia hawa viongozi na wakuu na ukawapendelea wao juu yetu ili utakapodhibiti mambo utarejea katika yaliyo bora kama alivyokuzoeza Mwenyezi Mungu katika kugawa kwa usawa, na kufanya uadilifu kwa raia." Akasema (as): "Je, mnaniamuru – ole wenu - nitake msaada na nusura kwa kuwatendea dhulma na uovu wale ambao nimetawalishwa kwao kati ya Waislamu!? Hapana Wallahi haitakuwa hivyo maadamu mwezi wachomoza na naona nyota mbinguni. Wallahi kama mali zao zingekuwa zangu ningefanya usawa baina yao, sasa itakuwaje na hali hii ni mali yao!?"[22]

Na walimjia wanawake wawili wote akawapa kwa usawa, walipoondoka mmoja wao akarejea na akasema: "Ewe Amirul-Muuminina! Mwenyezi Mungu amenipendelea kwa aliyokupendelea na

[20] Rejea iliyotangulia uk. 41.

[21] Rayshahariy: Muhammad, katika *Mausua'atul-Imam Aliyi Fil-Kitabi Wasunnah Wataarikh*, Juz. 4, uk. 194, Chapa ya kwanza 1421Hijiria, Darul- Hadith- Qum.

[22] Rejea iliyotangulia uk. 195.

kukutukuza!" Akasema: "Ni kwa lipi amenipendelea Mwenyezi Mungu na kunitukuza?" Akasema: "Kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww)." Akasema: "Umesema kweli. Na wewe ni nani?" Akasema: "Mimi ni mwanamke wa Kiarabu na huyu ni katika watumwa." Ali (as) akachukua udongo kutoka ardhini kisha akasema: "Nimesoma yaliyo baina ya vibao viwili, na sijaona katika kizazi cha Ismail ubora wowote walio nao juu ya kizazi cha Is'ahaq hata wa ubawa ya mbu."[23]

[23] Rejea iliyotangulia uk. 196.

# HAKI ZA WASIOKUWA WAISLAMU:

Imam Ali (as) alijali sana suala la kulinda haki za kila raia katika dola yake, Mwislamu au asiyekuwa Mwislamu, kwani asiyekuwa Mwislamu ni mshirika katika ubinadamu na uraia kama alivyosema (as): "Ama ni ndugu yako katika Dini au ni mfano wako katika kuumbwa (ni binadamu kama wewe)." Kwa sababu hiyo tunakuta Imam Ali (as) anaumia sana kwa kuvunjwa heshima ya mwanamke asiyekuwa Mwislamu kama anavyoumia kwa mwanamke wa Kiislam. Na anaona linapotokea jambo miongoni mwa hayo katika nchi ya Waislamu bila ya kupambana nalo au kuonya, hali hiyo inapokonya maisha thamani yake na inatosha kuwa ni sababu ya kuchagua mauti kwa majuto na masikitiko. Anasema (as) katika kukemea moja ya mashambulizi ya jeshi la Muawaiya:

**وَلَقَدْ بَلَغَنِي أَنَّ الرَّجُلَ مِنْهُمْ كَانَ يَدْخُلُ عَلَى المَرْأَةِ المُسْلِمَةِ، وَالْأُخْرَى المُعَاهَدَةِ، فَيَنْتَزِعُ حِجْلَهَا وَقُلْبَهَا وَقَلاَئِدَهَا، وَرِعَاثَهَا، ما تَمْتَنِعُ مِنْهُ إِلاَّ بِالْإِسْتِرْجَاعِ وَالْإِسْتِرْحَامِ، ثُمَّ انْصَرَفُوا وَافِرِينَ، مَا نَالَ رَجُلاً مِنْهُمْ كَلْمٌ، وَلاَ أُرِيقَ لَهُمْ دَمٌ،فَلَوْ أَنَّ امْرَأً مُسْلِماً مَاتَ مِن بَعْدِ هَذا أَسَفاً مَا كَانَ بِهِ مَلُوماً، بَلْ كَانَ بِهِ عِنْدِي جَدِيراً.**

**"Na habari zimenifikia kuwa mtu miongoni mwao huingia kwa mwanamke Mwislamu na mwanamke dhimiy na anampora pambo la mguuni, bangili, kidani chake, na shanga na hamuwezi kumzuia ila kwa kusema: 'Kwa hakika Sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na sisi ni wenye kurejea Kwake.' Na kupiga kelele ili kuomba kuhurumiwa, kisha wakaondoka bila ya kupungua mtu kati yao, wala hakuna aliyeje-**

**ruhiwa kati yao, wala kumwagika damu yao. Lau kama Mwislamu angekufa baada ya hali hii kwa majonzi, hangepaswa kulaumiwa, bali kwa mtazamo wangu angekuwa amestahiki!"**[24]

Na wakati mmoja Imam Ali (as) alimuona mzee mmoja kipofu, mkubwa kwa umri akipita huku akiwa anaomba, Amirul-Muuminina akasema: "Ni nani huyu?" Wakasema: "Ewe Amirul-Muuminina ni mkristo!" Amirul-Muuminina (as) akasema: "Mmemtumia hadi alipozeeka na akawa kikongwe ndipo mnamnyima? Mpeni kutoka Baitul-Mali."[25]

Na aliandika barua kwa watumishi wake kuhusu ukusanyaji wa kodi akisisitiza kuheshimiwa mali na haki za kila raia Mwislamu na asiyekuwa Mwislamu, anasema (as): "Wala msivunje heshima ya mali ya yeyote miongoni mwa watu wenye kuswali au wenye mkataba."[26] Na tunakuta kilele cha heshima na usawa mbele ya kanuni ambayo ameinukuu Ibnu Athiir katika kitabu chake *al-Kaamil Fiy Tarikh* kutoka kwa Sha'abiy, amesema: "Ali aliipata ngao yake kwa mkristo hivyo akampeleka kwa Kadhi Shurayh, akasema (as): 'Hii ni ngao yangu.' Mkiristo akasema: 'Si vinginevyo hii ni yangu. Na Amirul-Muuminina hakusema uongo.' Shurayh akamwambia Ali: 'Una ushahidi?' Akasema: 'Hapana." huku akicheka, basi mkiristo akachukua ngao na akatembea hatua chache, kisha akarejea na akasema: 'Nashuhudia kwamba hizi ni hukumu za Manabii! Amirul-Muuminina amenileta kwa Kadhi wake, Kadhi wake anahukumu dhidi yake kisha yeye anasalimu amri!' Na akakiri kwamba ngao ilidondoka kwa Ali (as) wakati wa kwenda kwake Siffin, Ali akafurahi kwa kusilimu kwake, na akampa zawadi ngao na farasi."[27]

---

[24] Al-Musawiy: Sharifu Ridhaa, katika *Nahjul-Balaghah*, Hotuba ya 27.

[25] Al-Musawiy, Sharifu Ridhaa, katika *Nahjul-Balaghah*, Hotuba ya 28.

[26] Al-Hurru al-Amiliy: Muhammad bin Hasan, katika *Wasailus-Shiah*, Hadith namba 19996.

[27] Ibnul-Athiyr, katika *Kaamilu Fiy Taarikh*, Juz. 2, uk. 443, Muasasatu Taarikhil-Arabiy – Beirut 1989.

# PAMOJA NA WAPINZANI WA RAI:

Wakati walipojitenga baadhi ya watu na Imam Ali, baada ya kadhia ya Hukumu huko Siffin, na wakatangaza upinzani wao kwa Imam (as) na kumkhalifu kwao katika rai yake, bali wakamtuhumu kwa ukafiri, na hao ni wale ambao wanajulikana kama Khawarij (Waasi), Imam (as) alikataa kuvunja haki zao za uraia na kufanya ubaguzi wa aina yoyote dhidi yao kwa upinzani wao katika rai ya kisiasa au ya kidini, maadamu tu hawajafanya jambo la kuhatarisha amani kwa kutumia silaha na mabavu. Na jambo zuri ni kwamba Imam Ali (as) alianza kutangaza haki zao mbele ya Ummah. Imekuja katika *Daaimul-Islam* na *Tarikh Ibnu Khalidun* kwamba: "Ali (a.s.) alihutubia huko Kufah, akasimama mtu kati ya Makhawarij akasema: "Hakuna hukumu isipokuwa ya Mwenyezi Mungu." Ali alinyamaza, kisha akasema mwingine na mwingine tena maneno hayo hayo. Walipozidisha kwake akasema (as): "Neno la haki linakusudiwa humo batili, mnayo mambo matatu kwetu: Hatuwazuii kuja msikitini na kuswali humo, wala hatuwanyimi pato maadamu mikono yenu ipo pamoja na mikono yetu wala hatutowaanza kwa vita hadi mtuanze."[28]

Na baada ya tukio la Nahrawan baadhi ya wafuasi wa Imam Ali walimsikia mtu anayeitwa Abul-Izaar Twaiy akiwa anadhihirisha rai ya Makhawariji, wakamleta kwa Imam Ali (as) wakisema: Hakika huyu ana rai ya Makhawariji, na wakanukuu maneno yake, akasema (as): "Nimfanyeje?" Wakasema: "Muuwe." Imam akasema: "Nimuuwe ambaye hanipigi vita?" Wakasema: "Mfunge." Akasema: "Hana hatia nitakayomfunga kwayo, mwacheni."[29]

---

[28] Rayshahariy: Muhammad, katika *Mausua'atul-Imam Aliyi Fil-Kitabi Wasunnah Wataarikh*, Juz. 6, uk. 342, Chapa ya kwanza 1421 Hijiria, Darul- Hadith-Qum.

[29] Al-Khatibu al-Baghidadiy, katika *Taarikh Baghdadiy*, Juz. 14, uk. 366, Darul-Kutubil-Ilimiya – Beirut.

Ummah wa Kiislam una haja kubwa katika zama hizi ambazo baadhi ya jamii zake zinaishi katika hali ya huzuni ya ukosefu wa usawa, fitina za kukhitalafiana za makundi na ukabila, kusoma sira ya Imam Ali (as) ili ujue utukufu wa mafunzo ya Uislamu, na kujiepusha kwake na wanayoyafanya kwa jina la Uislamu miongoni mwa dhulma na uovu. Ni haja kubwa ilioje kwetu kumsoma Ali (as) katika usawa na uadilifu, na kudhihirisha mfumo huu kimatangazo na kiutamaduni kwa kiwango cha kimataifa, ili kukabiliana na mashambulizi ya upotoshaji ambayo yanaulenga Uislamu na Waislamu, hususan kuanzia tarehe 11 Septemba, kwa ajili ya kumulika vita vya mgongano wa kiutamaduni baina ya utamaduni wa kimagharibi na wa Kiislam, kama yanavyopanga vita hivyo makundi ya ushawishi ya Kizayuni na Wakristo wa mrengo wa kulia wenye kuchupa mipaka, ili katika kivuli cha vita hii ya kutengeneza, Mazayuni waendeleze uvamizi wao kwa Wapalestina na kukandamiza harakati za wananchi wake wenye kupambana, na kutimiza tamaa zake pana za kiuadui.

# MUAMALA WA KIBINADAMU KATIKA SIRA YA IMAM ALI (AS)

Sira ya Amirul-Muuminina Ali (as) imesifika katika mambo mengi, yaliyo dhahiri zaidi ni muamala wake wa kibinadamu pamoja na wengine, uliojengeka juu ya msingi wa kuheshimu binadamu kama binadamu, kwa kuachilia mbali kitu kingine, na kuhifadhi juu ya haki yake na shakhsiya yake ya kimaada na kimaanawi popote na sehemu yoyote, na vyovyote itakavyokuwa ukubwa wake na kiwango chake. Na umuhimu wa mwelekeo wa upande huu katika sira ya Amirul-Muuminina (as) unatokana na nafasi yake katika kuathiri maisha ya binadamu kwa jumla, kiutu na kijamii, na katika kuwa kwake ni njia ya kuelekea kwenye radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mimi na wewe tunaamiliana pamoja na binadamu, ni sawa wakiwa wanaafikiana na sisi katika dini na mwelekeo au wanatofautiana na sisi. Na lililo muhimu katika sehemu hii, ni tujue namna ya kuamiliana pamoja nao kwa muamala mzuri wa kibinadamu, ambao unaakisi usafi wa Uislamu na kumheshimu binadamu kama binadamu kabla ya kupata sifa yoyote nyingine, inayoongeza kwake mazingatio mengine.

Sira ya Amirul–Muuminina (as) ilikuwa imejaa mifano mingi ya muamala wa kibinadamu pamoja na wengine, katika hali na mazingira mbalimbali. Naye kwa hakika baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww) ni mfano bora na kigezo cha kuiga. Na hakika kuwepo mtazamo huu katika maisha yake ndio ambao umefanya shakhsiya yake kuwa shakhisiya ya kibinadamu yenye kudumu katika kiwango cha binadamu wote, na sio katika historia ya Waislamu

peke yao. Na kabla ya siku chache imetoka diwani mpya ya mashairi huko Beirut ya mkiristo, naye ni Joseph Hashim, kuhusu Imam Ali, chini ya anwani *Alawiyaati*. Ama kitabu *al-Imamu Aliyu Swautul-Adalatil-Insaaniyah* cha mwanafasihi wa kikristo George Jardac ni rejea nzuri (Kimetarjumiwa kwa Kiswahili kwa jina la **Sauti ya Uadilifu ya Ubinadamu**), imechukua nafasi yake katika maktaba ya utamaduni na fasihi ya Kiarabu. Na vilevile rejea ya *Idul-Ghadiyr* cha mkiristo Paulo Salama, na vinginevyo miongoni mwa kazi za fasihi, kihistoria na kifikra, ambazo zinaeleza juu ya nafasi ya Imam Ali (as) katika kiwango cha ubinadamu.

# MAJI NI HAKI YA WOTE:

Miongoni mwa ushahidi wa muamala wa kibinadamu kwa Imam Ali (as) ni yaliyotokea katika vita vya Siffin, wakati jeshi la Muawaiya lilipolitangulia jeshi la Imam Ali kufika katika sehemu ya mapigano na kudhibiti sehemu ya maji ya Mto Furati na likalizuia jeshi la Imam Ali kwenda kwenye maji. Wafuasi wa Imam Ali (as) wakapiga kelele juu ya hilo, akasimama akawahutubia na akasema neno lake mashuhuri:

قَدِ اسْتَطْعَمُوكُمُ الْقِتَالَ، فَأَقِرُّوا عَلَى مَذَلَّةٍ، وَتَأْخِيرِ مَحَلَّةٍ، أَوْ رَوُّوا السُّيُوفَ مِنَ الدِّمَاءِ تَرْوَوْا مِنَ الْمَاءِ، فَالمَوْتُ فِي حَيَاتِكُمْ مَقْهُورِينَ، وَالْحَيَاةُ فِي مَوْتِكُمْ قَاهِرِينَ. أَلاَ وَإِنَّ مُعَاوِيَةَ قَادَ لُمَةً مِنَ الْغُوَاةِ وَعَمَّسَ عَلَيْهِمُ الْخَبَرَ، حَتَّى جَعَلُوا نُحُورَهُمْ أَغْرَاضَ الْمَنِيَّةِ.

**"Kwa hakika wamekuombeni vita, basi bakieni katika madhila na kubaki nyuma kwa daraja (ikiwa hamutoshiriki vita), au zikozeni kiu panga kwa damu mtakoza kiu zenu kwa maji. Mauti hasa ni maisha ya kuburuzwa, na uhai hasa ni kufa ndani ya kutenzwa nguvu. Lo! Kwa hakika Muawiya ameongoza kikundi cha watu waasi na amewafichia kheri kiasi cha kuzifanya shingo zao kuwa kusudio la mauti."**[30]

Imam kwa hilo akaliamsha jeshi lake ili kufika kwenye maji na haya ndio yaliyotokea hasa, ambapo waliweza kuliondoa jeshi la Muawiya kwenye maji na hatimaye wakayadhibiti wao, ilipoku-

[30] Al-Musawiy, Sharifu Ridhaa, katika *Nahjul- Balaghah*, Hotuba ya 51.

wa hivyo watu wakapiga kelele wakimwambia: "Tuwanyime maji kama walivyotunyima na tuwauwe kwa panga za kiu." Lakini yeye alikataa hilo na akasema: "Chukueni mahitaji yenu katika maji na rejeeni kwenye kambi yenu na waachieni maji, hakika mimi sifanyi waliyoyafanya wajinga."[31]

Hivi ndivyo anavyotupigia mfano wa kuigwa katika kukataa kutumia vikwazo, kibano na kumnyima mahitaji ya dharura ya maisha adui ambaye anapigana naye vita kali hata kama adui atakimbilia kwenye mbinu hii. Kwa hakika hii ni tabia ya Kiislamu katika upeo wake mkubwa wa kibinadamu. Na unapotafuta mtazamo huu katika uhalisia wa ulimwengu wa kimataifa, utakuta kwamba haupo katika kamusi ya siasa ya kimataifa ya leo. Ndio maana unaona dola kubwa na zenye udhibiti zinatumia vikwazo dhidi ya wananchi dhaifu kwa hoja ya kumaliza upinzani wao na upinzani wa baadhi ya mifumo na tawala, licha ya kwamba wao wanajua vizuri kwamba waathirika wa vikwazo hivi ni wananchi wenyewe.

Marekani na dola za Magharibi zilipowawekea vikwazo wananchi wa Iraki, wao walikuwa wanajua kwa yakini kwamba havitobadilisha chochote katika ubabe wa utawala wa Iraki na wala havitopelekea kwenye mabadiliko ya kisiasa, bali kinyume cha hivyo vitaongeza udhaifu katika msimamo wa wananchi dhidi ya utawala, kwa sababu lengo lao litakuwa ni kupata chakula na riziki. Ama utawala hakika utafaidika na hali hii katika kuweka kanuni ya kudhibiti mamlaka yake, na kupanua maslahi yake. Na kupitia vikwazo vilivyowekwa utapata mada ya propaganda ya kupambana na uadui wa nje, na kubakisha hali ya hatari isiyotangazwa na kisha kukandamiza kila upinzani.

Je, amedhurika mtawala wa zamani wa Iraki kutokana na vikwazo? Je, watoto wanaokufa kwa sababu ya upungufu wa madawa na

[31] Al-Qazuwiniy, Sayyid Muhammad Kadhim katika *Aliyu Minal-Mahadi Ilallahdi*, uk, 334, Chapa ya al- Adab - Najaf tukufu 1967.

chakula ni watoto wa Rais aliyeondolewa au wa mawaziri au wa maafisa wa juu wa jeshi? Hakika wamagharibi wanajua kwamba watoto ambao wanakufa kutokana na vikwazo, hakika wao ni watoto wa watu mafakiri na wasio na kitu. Ama watoto wa vigogo hakika hawazaliwi isipokuwa na katika vinywa vyao kuna kijiko cha dhahabu kama inavyosemwa.

Wamagharibi wameiwekea Libya vikwazo miaka mingi kwa matatizo yake na utawala, na tumeona wanatumia nguvu zaidi ya hiyo dhidi ya Sudan hadi mambo yamefikia kupiga na kubomoa viwanda vya dawa katika nchi masikini inayokabiliwa – kabisa – na upungufu mkubwa katika sekta hii, na ambayo baadhi ya wananchi wake wanakufa kwa sababu ya upungufu mkubwa wa madawa na kwa sababu ya lishe mbaya. Uko wapi ubinadamu katika yote haya, je, hiyo si dalili juu ya kutoweka kwa upeo wa ubinadamu katika fikra ya utamaduni wa kimagharibi na mtazamo wake katika maisha? Lakini tunaukuta utamaduni wa Kiislamu na vielelezo vyake ukiwa kinyume cha hayo.

# HATA MHAINI ANA HAKI ZAKE:

Na miongoni mwa ushahidi katika sira ya Ali (as) ni kisa hiki muhimu: Mtu mmoja aliyekuwa mfuasi wa Imam (as) jina lake ni Ubaidullahi bin al-Hurru al-Ja'afiy, alimsaliti Imam (as) na akajiunga na jeshi la Muawiya wakati wa usiku, na hiyo ni wakati vita vya Siffin vikiwa vimepamba moto. Na katika kanuni za vita mhaini kama huyu anapasa kuadhibiwa kwa kunyongwa. Ubaidullahi aliweza kutoa msaada mkubwa kwa Muawaiya. Ama mke wake alikuwa huko Kufah, na alisikia habari za kufariki kwa Ubaidullahi vitani, hivyo akakaa eda ya kufiwa, na baada ya hapo akaolewa na mwanaume wa Kufah, wakati ambapo Ubadullahi alikuwa angali hai huko Sham. Alipopewa habari ya mke wake kuolewa alitoka usiku na akasafiri masafa marefu hadi Kufah, aliingia usiku na haraka alielekea kwenye nyumba ya mke wake. Mke wake alitoka akiwa amevaa nikabu, na baada ya majadiliano mafupi alimpa habari ya kuolewa kwake na mtu mwingine.

Ubaidullahi akaona milango ya kurejea kwa mke wake imefungwa mbele yake, na akaona utatuzi bora ni kuonana na Amirul-Muuminina (as) na amwambie kisa chake, Amirul-Muuimina ni mtu wa uadilifu na haki, na wala hapindishi haki hata kama mwenye haki ni mhaini. Ubaidullahi alikutana na Amirul-Muuminina (as) hali ya kuinamisha kichwa kwa aibu kwa kujua kwake kwamba ni mhaini. Alimsalimu Imam (as), Imam akamwitikia na akamuuliza: "Wewe si Ubaidullahi? Eee wewe ni mnafiki uliomsaliti Imam wako na dini yako na ukajiunga na safu ya ukafiri na unafiki katika mazingira ya vita. Je, wewe ndio mtu huyo?"

Ubaidullahi anajua kwamba Ali ni mtu wa haki na uadilifu, hivyo alitumia fursa hii na akasema: "Je, usaliti wangu unakuzuia kufanya

uadilifu ewe Amirul- Muuminina?" Imam akamjibu: "Vipi?" Na akamwomba amwelezee kisa chake, alimwelezea na akamtaka Imam amsaidie katika jambo lake. Imam (as) akaamrisha kuletwa mke wake na mume wake wa pili na akamwambia mwanamke ajitenge na mume wake wa pili na aanze kukaa eda kuanzia sasa. Na baada ya kumalizika eda arejee kwa mume wake wa kwanza kama atakuwa sio mjamzito, na ikiwa ni mjamzito mume wa kwanza hatomrejea hadi ajifungue, na mtoto wake ni wa halali na atamfuata baba yake, yaani mume wa pili, na baada ya hapo mke atarejea kwa mume wake wa kwanza.

Na inafaa kutaja kwamba mke ambaye mume wake ametoweka kama atairejea Mahakama ya Kiislamu ya kisharia na hakimu akampa talaka ya kisharia, kisha akarejea mume wa kwanza, hawezi kumrejea na wala haitenguki ndoa ya mume wa pili, nayo ndio sahihi. Ama mke wa Ubaidullahi hakuirejea Makahama ya Kiislamu bali yeye mwenyewe alikaa eda na kuolewa, na kwa sababu hiyo imevunjika ndoa ya pili baada ya kufika mume wa kwanza kwa urahisi na bila ya talaka.[32] Hakika uadilifu ni sharia madhubuti haivunjiki hata katika kuamiliana na adui, na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ ۖ وَلَا
يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَآنُ قَوْمٍ عَلَىٰ أَلَّا تَعْدِلُوا ۚ اعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ
لِلتَّقْوَىٰ ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ

[32] Shiraziy: Sayyid Muhammad, katika *al-Hukumatul-Islamiya Fiy Ahdi Amirul-Muuminina*, Muasasatul- Fikril-Islamiy, uk. 69, Chapa ya kwanza.

**“Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mtoao ushahidi kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusiwapelekee kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu ndiko kunakokurubisha kwenye takua. Na Mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyatenda.” (Surat Maida: 8).**

# KUCHUKIA KUADHIBU:

Sira ya Imam Ali (as) imejaa ushahidi na visa ambavyo vinatia mkazo wa kuheshimu kwake ubinadamu wa mwanadamu na kulinda kwake heshima na utu wake, Imam (as) alijiwa na mwanamke akasema: "Hakika mume wangu amemwingilia kijakazi wangu bila ya idhini yangu." Imam (as) akamuuliza mume: "Unasemaje?" Akasema: "Sikumwingilia isipokuwa kwa amri yake." Akasema (as) kwa kumwelekea mwanamke: "Ikiwa wewe ni mkweli basi nitampiga mawe na ikiwa wewe ni muongo basi tutakuadhibu (atapigwa viboko kwa kusema uongo)." Swala ikakimiwa Imam Ali akasimama kwa ajili ya kuswali. Mwanamke akatafakari katika nafsi yake hakuona faraja mume wake kupigwa mawe wala yeye kuadhibiwa, akatoka na hakurudi, na Ali (as) hakumuulizia. Wakati ambapo Imam (as) alikuwa anaweza kuamuru akamatwe na kuletwa, na kumleta mume wake na kuadhibiwa mmoja wao, lakini yeye (as) alikuwa anachukia kutoa adhabu pamoja na kulinda haki na utaratibu, hakuwa anabeba katika maamuzi ya nafsi yake hali ya kupenda kuadhibu watu na alikuwa anasamehe kadiri ya uwezo wake."[33]

[33] Shiraziy: Sayyid Muhammad, katika al-Hukumatul-Islamiya Fiy Ahdi Amirul- Muuminina, Muasasatul- Fikril-Islamiy, uk. 23, Chapa ya kwanza.

# KUMFANYIA WEMA MHALIFU:

Ama sura nzuri ya hali ya ubinadamu katika maisha ya Imam Ali (as) imedhihirika katika saa za mwisho za maisha yake matukufu, alipoamiliana na mtu ambaye alimpiga kwa upanga akiwa kwenye mihrabu ya Swala yake. Abdur-Rahman bin Muljim alikimbia msikitini akitaka kutoroka isipokuwa kelele zilipaa katika anga la Kufah na watu wengi walitoka katika nyumba zao kumtafuta muuwaji, na hivyo njia na vichochoro vyote vya Kufah vikazibwa mbele ya Ibnu Muljim hadi baadhi ya wafuasi wa Ali (as) wakamkamata, wakamleta kwake naye akiwa angali hai ameathirika na pigo la upanga wenye sumu na damu zinavuja katika kichwa chake. Na wafauasi wake wakipiga kelele; huyu hapa adui wa Mwenyezi Mungu tumekuletea ewe Amirul-Muuminina. Imam (as) alimwangalia kwa jicho la huruma na sio mtazamo wa kulipa kisasi na akamwambia: "Ewe Ibnu Muljim! je nilikuwa Imam mbaya kwako?" Ibnu Muljim akawa analia na kusema: "Hapana, lakini je, wewe utamuokoa ambaye yuko katika moto?"

Ukaendelea muamala wake mzuri wa kibinadamu pamoja naye hadi katika pumzi yake ya mwisho ya maisha yake. Matabibu waliposema kwamba maziwa (mtindi) ndio dawa na chakula kwa ajili ya Imam (as) watu walijitolea hadi mafakiri na wasio na kitu wa mji wa Kufah walileta maziwa kadiri wawezavyo kwenye nyumba ya Imam Ali, alipokunywa kidogo alimpa mtoto wake yaliyobakia katika kikombe na akasema: "Mpelekee mateka wenu mlisheni katika mnavyokula na mnywesheni katika mnavyokunywa, mtunzeni vizuri mateka wenu."

Sio ajabu lile wanaloliitakidi baadhi ya watu kwamba kama Imam (as) angepona na kuendelea kuishi angemsamehe Ibnu Muljim. Na haya yananasibiana na msamaha wa kudumu wa Imam (as).

# AU KUSAMEHE DHAMBI:

Hakika hiki ni kiwango cha juu cha ubinadamu ambacho kilikuwa katika shakhisiya ya Ali, nacho ndicho kilichomnyanyua Ali (as) katika daraja za utukufu unaodumu milele, ni nadra kupata mfano wake isipokuwa kwa mwalimu wake na mkufunzi wake Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww). Imepokewa kwamba yeye (as) alikuwa amekaa na wafuasi wake akapita mbele yake mwanamke mzuri, watu wakamtazama kwa macho yao, akasema (as) "Hakika macho ya mafahali hawa yanatamaa, na hakika hiyo ni sababu ya kuangamia kwao. Anapotazama mmoja wenu mwanamke na akamvutia, basi amwendee mke wake hakika yeye ni mwanamke kama alivyo mke wake." Mtu katika Makhawariji akasema: "Mwenyezi Mungu amlaani kafiri huyu anajua nini?" Watu wakamrukia ili wamuuwe. Akasema (as): "Pole pole, hakika ni tusi kwa tusi au kusamehe dhambi."[34]

Na katika sira ya Imam Ali (as) tunaweza kujifunza mengi na kushikamana na mengi miongoni mwa mitazamo mitukufu, na kudumu katika shakhisiya yake, isipokuwa kuelewa upeo wa ubinadamu katika maisha yake kunabakia kuwa ni jambo umuhimu zaidi na la kusisitizwa zaidi, kwani wakati ambapo mwanadamu anapata maendeleo yenye kushangaza katika nyanja nyingi za maisha yake, anaweza kughafilika kwamba furaha yake katika maendeleo yake hayo haitokamilika kama utakosekana upande huu (wa ubinadamu na utu).

[34] Al-Musawaiy: Sharifu Ridhaa, katika Nahjul-Balagha, Hekima namba 420.

# BIBLIOGRAFIA

- Al-Alusiy: Sayyid Mahmud, katika *Ruhul-Ma'aniy Fiy Tafsril-Qur'an*, Chapa ya nne Daru Ihiyaai Turathil-Arabaiy – Beirut 1985.

- Ibnul-Hadid: Abdul-Hamid, katika *Sharhu Nahjul-Balagha*, Chapa ya kwanza 1987 Darul-Jiyl – Beirut.

- Ibnul-Athiir, katika *Kaamilu Fiy Taarikh*, Muasasatu Taarikhil-Arabiy – Beirut 1989.

- Ibnu Hanbali: Imam Ahmad, *Musnad Imam Hanbal*, Alamul-Kutubi – Beirut 1998.

- Ibnu Sa'ad, *Twabaqaatul-Kubraa*, Daru Swaadir – Beirut 1989.

- Bukhariy: Muhammad bin Ismail, katika *Sahih Bukhariy*.

- Ibnu Majah al-Qazuwiniy: Muhammad bin Yazid, katika *Sunanul-Kubraa* ya Ibnu Maajah, katika mlango wa Fadhila za Ali.

- Al-Hakim Nisaburiy: Muhammad bin Abdillahi, katika *Mustadrak Alas-Sahihayn*.

- Al-Hurru al-Amiliy: Muhammad bin Hasan, katika *Wasailus-Shiah*.

- Husain: Dkt. Twaha, katika *Fitinatul-Kubraa*.

- Al-Khatibu al-Baghidadiy, katika *Raarikh Baghdadiy*, Darul-Kutubil- Ilimiya – Beirut.

- Al-Khatibu: Abdul-Karim, katika *Ali bin Abi Twalib Baqiyatun-Nubuwah Wakhatamil-Khilafah*, Darul-Ma'ariafa – Beirut 1975

- Rayshahariy: Muhammad, katika *Mausua'atul-Imam Aliyi Fil-Kitabi Wasunnah Wataarikh*, Chapa ya kwanza 1421Hijiria, Darul-Hadith - Qum.

- Sarkhisiy: Shamsu Diyn, katika *al-Mabusut*, Darul-Maarif - Beirut 1406 Hijiria.

- Shawkaaniy: Muhammad bin Ali, katika *Fat'hul-Qadiyr*, Chapa ya al-Asriya Swaida – Beirut 1997.

- Shiraziy: Sayyid Muhammad, katika *al-Hukumatul-Islamiya Fiy Ahdi Amirul-Muuminina*, Muasasatul- Fikril-Islamiy, Chapa ya kwanza.

- Swaalihiy Shaamiy: Muhammad bin Yusuf, katika *Subulul-Hudaa Warashaadiy-Fiy Sirati Khairil-Ibaad*, Chapa ya kwanza 1993, Darul-Kutubil-Ilimiya – Beirut.

- Tabari: Muhammad bin Jarir, katika *Taarikh Tabariy*.

- Al-Qazuwiniy: Sayyid Muhammad Kadhim, katika *Aliyu Minal-Mahdi Ilallahdi*, Chapa ya al-Adaab – Najaf al-Ashraf 1967.

- Al-Qushayriy: Muslim bin al-Hajaj, katika *Sahih Muslim*.

- Al-Kayaaliy: Abdul-Wahab, katika *Mausuatu Siyasah*, Chapa ya kwanza 1986, Musasatul-Arabiya Lilidiraasati Wanashir – Beirut.

Al- Musawiy: Sharif Ridhaa, katika *Nahjul-Balagha*.

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

## AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa

17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.

39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata

60. Umaasumu wa Mtume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)

81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi

103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsaalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa

125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.

168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye

189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwanendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu na vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja’aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii

210. Maadili ya Ashura

211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi

212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza

213. Imam Ali na Mambo ya Umma

214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi